# Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

## 1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 JANUARI, 2026 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 JANUARI, 2026.

### 1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 11-20 JANUARI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilidumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini zaidi na kuwepo katika maeneo ya magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) lilikuwa la chini ya wastani. Hali hii ilidhoofisha mifumo isababishayo mvua (ITCZ) katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu na maeneo ya Nyanda za juu kaskazini mashariki. Hata hivyo, vipindi vichache vya upepo uvumao kutoka baharini viliimarisha mifumo isababishayo mvua nyepesi katika maeneo hayo.

### 1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 JANUARI, 2026.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea uwepo wa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, Kati, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi, na mvua nyepesi katika maeneo ya ukanda pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki.

## 2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-31 JANUARI, 2026.

### 2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 JANUARI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

kudumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya magharibi mwa nchi yetu, nyanda za juu kusini magharibi na kusini. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kudhoofisha mifumo isababishayo mvua (ITCZ) katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu, Nyanda za juu kaskazini mashariki na maeneo jirani.

**2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 JANUARI, 2026.**

**Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Mvua zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Imetolewa na:

***MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA***

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz